je ninaweza kukuuliza swali

Je, kuna yeyote
aliyewahi
kuchukua
Biblia
na kukuonesha
jinsi unavyoweza

KUJUA

kwa hakika kwamba
utaenda mbinguni?

Biblia ina

HABARI MBAYA

na pia

HABARI NJEMA.

Habari mbaya ni jambo linalokuhusu **WEWE**.

Habari njema ni jambo linalomhusu **MUNGU**.

Hebu tuangalie habari mbaya kwanza…

Habari Mbaya 1

Zote tu wenye dhambi.

Warumi 3:23 yasema *"Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa—na utukufu wa Mungu."*

"Mwenye dhambi" ina maana ya kwamba tumekosa shabaha. Tunapodanganya, tunapochukia, tunapokuna na tamaa mbaya, ama tunaposengenya, na tunapokosa kanuni Mungu aliyoweka.

Fikiria kama mimi na wewe tungepaswa kila moja kurusa jiwe na kujaribu kupiga ncha ya kaskazini. Unaweza kurusa mbali zaidi kuliko mimi, lakini hakuna hata mmja kati yetu atakayeigonga.

Biblia inaposema “Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa” ina maana kwamba sote tumepungukiwa na kipimo cha ukamilifu wa Mungu.

Katika mawazo, maneno na matendo, hatukuwa wakamilifu. **Lakini habari mbaya inazidi kuwa mbaya zaidi...**

Habari Mbaya 2

Adhabu wa dhambi ni mauti.

Warumi 6:23 yasema, *"Mshahara wa dhambi ni mauti."*

Iwapo nimekuajiri kunifanyia kazi na nikakulipa KSH 50, huo ndio mshahara wako. Hicho ndicho ulichopata.

Biblia inasema kwamba tunapotenda dhambi tunavuna mauti. Ina maana kwamba tunastahili kufa na kutengwa na Mungu milele.

Lakini...

kwa sababu haikuwepo njia kwetu kumfikia Mungu, Biblia yasema Mungu alikuja kwetu.

Habari Njema 1

Kristo alikufa kwa ajili yako.

Warumi 5:8 yatuambia, *"Mungu alidhihirisha upendo wake kwetu kwa vile tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu."*

Fikiria umelazwa hospitalini unaposubiri kufa kwa sababu ya ugonjwa wa saratani. Ikiwa nitakujia na kusema "Hebu tuondoe chembechembe za saratani mwilini mwako na tuziweke mwilini mwangu."

Kama hiyo inawezekana,

- **Nini kitakachotokea kwangu?**
- **Nini kitakachotokea kwako?**

Nitakufa nawe utahishi.

Nitakufa kwa niaba yako.

Biblia inasema Kristo alichukua adhabu tuliyoistahili kwa sababu ya dhambi, akaiweka juu yake mwenyewe, na akafa mahali petu. Siku tatu baadaye Kristo alitoka kuzimu kuthibitisha kwamba dhambi na mauti vimeshindwa na ya kuwa madai yake kwamba ni Mungu yalikuwa ya kweli.

Kadiri habari mbaya ilivyokuwa mbaya zaidi, habari njema ilikuwa nzuri zaidi!

Habari Njema 2

Unaweza kuokolewa kwa njia ya imani katika Kristo.

Waefeso 2:8-9 yasema, *"Kwa maana mmeokolewa (kukombolewa kutoka mshahara wa dhambi) kwa neema (upendeleo usiostahili), kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu; ni kipawa cha Mungu, wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*

Imani ina maana ya kutumaini.

S: Ni nini kinachokupasa kumwamini Kristo?

J: Inakupasa kumtegemea yeye pekee kukusamehe na kukupa uzima wa milele.

Kama jinsi unavyoweza kukitegemea kiti kukubeba bila jitihada yoyote kutoka kwako, kwa hiyo inakupasa kumwamini Yesu Kristo ili akufikishe mbinguni bila kutumia nguvu zako mwenyewe. Lakini unaweza kusema,



“Mimi ni mtu wa dini.”

"Mimi siibi."

"Mimi ni mtu mzuri."

"Mimi huenda kanisani."

"Ninawasaidia maskini."

Haya yote ni matendo mazuri; lakini kuishi vizuri, kuenda kanisani, kuwasaidia maskini au mambo mengine mema unayoweza kuyafanya kamwe hayatakufikisha mbinguni. Inakupasa kumwamini Kristo pekee, na Mungu atakupa uzima wa milele kama kipawa! Je, hili linaleta maana kwako?

Je, kuna kitu chochote kinachokuzuia kumwamini Kristo sasa hivi?

1. _____

2. _____

3. _____

4. _____

Ebu fikiria kwa makini. Hakuna chochote kilicho cha maana sana kuliko hitaji lako la kumwamini Kristo. Je, ungependa kumwambia Mungu ya kuwa **unamwamini Yesu Kristo kama mwokozi wako?** Kama ungetaka, kwa nini usiombe hivi sasa na kumwambia Mungu ya kuwa unamwamini mwanawe?

Kumbuka!

Si maombi yanayokuokoa. Ni kumwamini Yesu Kristo kunakokuokoa. Kuomba ni njia tu ya kumweleza Mungu kile unachofanya.

"Ee Mungu, mimi ni mwenye dhambi Ninajua dhambi zangu zinastahili adhabu. Ninaamini Kristo alikufa kwa ajili yangu na akafufuka na kutoka kaburini. Ninamwamini Yesu Kristo pekee kama Mwokozi wangu. Nakushukuru kwa msamaha na uzima wa milele nilivyonavyo sasa. Katika jina la Yesu, amen."

Ni kitu gani kimetendeka?

Yohana 5:24 inafasiria, *"Amin, amin, nawaambia, yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mauti kuingia uzima."*

» Je, "***umesikia***" neno la Mungu?
» Je, "***umeamini***" yale Mungu aliyosema na kumwamini Yesu kama Mwokozi wako?
» Je, "***ana uzima wa milele***" ina maana baadaye au sasa?
» Je, inasema "***hataingia hukumuni***" au inawezekana hataingia?
» Je, inasema "***amepita kutoka mauti***" au atapita?

Uzima wa milele una msingi juu ya uhakika, siyo juu ya hisia.

Kariri Yohana 5:24 leo.

Unafanya nini sasa?

Baada ya kumtumaini Kristo kama njia pekee ya kwenda mbinguni, hivi ndivyo unavyoweza kukua katika uhusiano wako naye.

» **Mwambie Mungu** yale yaliyomo moyoni mwako kwa njia ya maombi (Fil. 4:6,7).

» **Soma Biblia** kila siku, kujifundisha habari zake kutoka kwake (2 Timotheo 3:16-17). Anza na kitabu cha Wafilipi.

» **Abudu pamoja** na watu wa Mungu katika kanisa lililo karibu nawe (Waebrania10:24-25).

» **Waambie wengine** habari za Yesu (Math. 4:19).

Ikiwa umeona kipeperushi hiki kuwa cha msaada, tafadhali mshirikishe mwingine.

Kama una maswali zaidi kuhusu yaliyomo katika kipeperushi hiki, afikiana na:

Evantell

The Gospel. Clear and Simple.

p.o. box 741417 | dallas, tx 75374
www.evantell.org | 800.947.7359

© 2007 evantell, inc.

Kiswahili
TRMSW001